# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 14 MACHI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, JENIPHER NZOBE**

Kwa wiki inayoishia tarehe 14 Machi 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yalipungua kwa asilimia 60.25 kutoka TZS 13 bilioni hadi TZS 5.18 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kilipungua pia kwa asilimia 46.09 kutoka hisa milioni 5.5 hadi hisa milioni 2.99.

Jumla ya Mtaji wa Soko uliongezeka kwa asilimia 0.2 kutoka TZS 19.19 trilioni hadi TZS 19.22 trilioni. Mtaji wa Soko la Ndani uliongezeka kwa asilimia 0.14, hadi TZS 12.79 trilioni kutoka TZS 12.80 trilioni kutokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za DSE.

TBL imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 3.4 bilioni, ambayo ni 65.63% ya mauzo yote ikifuatiwa na CRDB kwa asilimia 26.26 ya mauzo yote.

Kuhusu bei, hisa za DSE ziliongezeka kwa TZS 20 wakati za NICO zikipungua kwa TZS 110 huku za TCCL nazo zikipungua kwa TZS 40.

CRDB iliongoza kwa idadi ya kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 59.95 sawa na hisa milioni 1.79 ikifuatiwa na Vodacom kwa asilimia 16.9. Jumla ya hisa milion 1.189 za NMB, Vodacom, TPCC na TBL ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa nje wakipungua wiki hii kulinganisha na wiki iliyopita. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 140 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 171 bilioni.

Mnada wa dhamana za muda mfupi za Serikali (T-Bills) uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 12 March 2025, ulifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 10.79 bilioni kwa dhamana za siku 35 na za siku 364.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA MACHI 14, 2025. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI JENIPHER NZOBE**